

03-Herufi Saba Na Viraa-a Saba

Maana ya Harf حرف Kilugha:

a) Neno au herufi kama vile herufi za Alfabeti au Abjadi.

b) Ukingoni mfano kama Anavyosema Allaah (سبحانه وتعالى):

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ

Na mionganini mwa watu yuko anayemwabudu Allaah ukingoni. [Al-Hajj: 10]

c) Kupindisha, kugeuza; mfano kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) kuhusu Mayahudi:

يُحَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَنْ مَوَاضِعِهِ وَنَسُوا حَظًا مِمَّا ذَكَرُوا

بِهِ

Wanageuza maneno (ya Allaah) kutoka mahali pake na wakasahu sehemu ya yale waliyokumbushwa. [Al-Maa'idah: 13]

d) Njia au kuelekea njia.

Neno la 'Harf' (moja) au 'Ahruf' (wingi) halijapatikana tarjuma yake halisi katika Sayansi ya Qur-aan. Kwa hiyo kwa usalama wa maana yake, tunalitaja kwa tamshi lake kama lilivyo. Lakini inaweza kufafanuliwa kwa kumaanishwa kuwa Harf au Ahruf ni lahaja za lugha ya Kiarabu kutoka makabila mbalimbali katika zama za Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ), na hivyo basi ni njia tofauti ambazo Aayah za Qur-aan zinasomwa. Mfano ukisema "Harf ya 'Aliy bin Abiy-Twaalib (رضي الله عنه)" inamaanisha kuwa unasoma Aayah

au neno hilo kwa jinsi ya Aliy bin Abiy-Twaalib (رضي الله عنه) alivyosoma Aayah hiyo au alivyotamka neno hilo.

Qur-aan iliteremshwa kwanza kwa Harf moja, kisha ikateremshwa kwa Ahruf nyinginezo zikawa ujumla ni Ahruf Sab'ah (saba) kwa sababu Waarabu walitofautiana kidogo lahaja zao.

Dalili ni Hadiyth ya Ibn 'Abbaas (رضي الله عنهمَا) ambaye amesimulia kwamba Nabiy (صلى الله عليه وآلہ وسلم) amesema:

((أَقْرَأَنِي جِبْرِيلُ عَلَى حَرْفٍ فَرَاجَعْتُهُ فَلَمْ أَزِلْ أَسْتَرِيدُهُ وَيَزِيدُنِي حَتَّى انتَهَى إِلَى سَبْعَةِ أَحْرَفٍ))

((Jibriyl alinisomea kwa Harf moja, nikaifanyia marudio mpaka akanifundisha nyingine, nikaendelea kumuomba nyinginezo mpaka mwishowe zikawa Ahruf Sab'ah [lahaja saba])) [Al-Bukhaariy, Muslim, Ahmad]

Ahruf Sab'ah hizo zilitokana na lahaja za makabila ya Quraysh, Hudhayl, Thaqiyf, Hawaazin, Kinaanah, Tamiym na Yeman. Kutofautiana kwake kulikuwa katika aina au njia saba:

1) Kubadilika neno.

Mfano:

عِبَاد

Imeandikwa kwa alif muhaqqaq (halisi) isipokuwa katika Suwrah Az-Zukhruf:

وَجَعَلُوا الْمَلِئَكَةَ الَّذِينَ هُمْ عِبْدُ الْرَّحْمَنِ إِنَّا

Viraa-a vinginevyo vya Naafi', Ibn 'Aamir, ibn Kathiyr, Abuu Ja'far wanasoma:

عِنْدَ

2) Tofauti ya neno au herufi.

Mfano katika Suwrah Al-Faatihah:

مُلِكٌ يَوْمَ الْدِينِ ۝

Neno la "Maalik" wengine wanalitamka: مَلِكٌ Maliki.

3) Kutangulizwa au kuweka nyuma neno.

Mfano kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى):

وَقُتْلُوا وَقُتِلُوا لَا كَفِرَنَ عَنْهُمْ سَيِّاتِهِمْ وَلَا دِخْلَنَهُمْ جَنَّتٌ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا أَلَّا هُرُثٌ ثَوَابٌ مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ وَاللَّهُ عِنْدَهُ حُسْنُ الْثَّوَابِ

Wakapigana na wakauliwa; bila shaka Nitawafutia makosa yao na bila shaka Nitawaingiza Jannaat zipitazo chini yake mito, ni thawabu kutoka kwa Allaah. Na kwa Allaah kuna thawabu nzuri kabisa. [Aal-'Imraan: 195]

Katika Qiraa-a cha Imaam Hamzah, Kisaaiy na Khalaf Al-'Aashir maneno mawili ya mwanzo yanasmwa:

وَقُتْلُوا وَقُتِلُوا

Wakauliwa na wakapigana.

4) Kupunguka au kuzidika neno.

Mfano kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى) ambayo Qiraa-a chetu cha Hafsw 'an Aaswim tunaisoma bila ya kihuishi cha من تَحْتَها kabla ya neno la

وَالشَّيْقُونَ الْأَوْلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالذِّينَ اتَّبَعُوهُمْ يَلْحَسِنُ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ
وَرَضُوا عَنْهُ وَأَعْدَّ لَهُمْ جَنَّتَ تَحْتَهَا الْأَنْهَرُ خَلِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ذَلِكَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

Na wale waliotangulia awali (katika Uislamu) mionganoni mwa Muhajirina na Answaar na wale waliowafuata kwa ihsaan; Allaah Ameridhika nao, nao wameridhika Naye. Na Amewaandalia Jannaat zipitazo chini yake mito, ni wenye kudumu humo abadi. Huko ndiko kufuzu adhimu. [At-Tawbah: 100]

Ama Imaam Ibn Kathiyr anaisoma kwa kihusishi hicho

مِنْ تَحْتِهَا

hivyo basi herufi hiyo ya ت inabadilika kwa kutamkwa kwa kasrah.

5) Kubadilika muundo wa neno.

Mfano:

سِرَاجًا

Kuna sehemu imeandikwa kwa alif muhaqqaq isipokuwa Suwrah Al-Furqaan imeandikwa kwa alif ndogo

سِرَاجًا

Riwaayah nyengine inasomwa kwa muundo wa wingi:

سُرُجًا

6) Muundo wa tamko kubadilika.

Mfano:

وَإِذْ جَعَلْنَا الْبَيْتَ مَثَابَةً لِلنَّاسِ وَأَمْنَا وَأَنْخَدُوا مِنْ مَقَامِ إِبْرَاهِيمَ مُصَلَّى

Neno hilo hapo la:

وَأَنْخَدُوا

ni amrisho, lakini Imaam Naafi' na Ibn 'Aamir wanasoma kwa kitenzi cha wakati uliopita:

وَاتَّخِذُوا

7) Tofauti ya kutamka.

Mfano yanavyotamkwa maneno yafuatayo kwa 'imaalah (kuinamisha au kuelekeza upande). Kuna imaalah al-kubraa (kuelemea kukubwa) na imaalah as-sughraa (kuelemea kudogo).

موسى التوراة والضحى

Muwsaa inatamkwa Muwsee. At-Tawraah inatamkwa At-Tawree. Wadhw-Dhwuhhaa inatamkwa Wadhw-Dhwuhee.

Mfano pia katika Aayah:

﴿وَقَالَ أَرْجُبُوا فِيهَا بِسْمِ اللَّهِ مَحْرُنَّهَا وَمُرْسَلَهَا إِنَّ رَبِّي لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ﴾

Qiraa-a cha Hafsw 'an Aaswim tunaschosoma sisi neno la

محرّنها

Tunaelemeza upande kwa kutamka: "majreehaa". Viraa-a vingine wanatamka kwa fat-hah au kasrah.

Lakini hali zote hizi aidha hazikubadilisha maana yake, au haziku haribu kusudio la kauli ya Allaah (سبحانه وتعالى).

Kuteremshwa Qur-aan kwa Ahruf Sab'ah kuliwafanyia sahali makabila ya Waarabu katika usomaji wa Qur-aan na kuihifadhi. Tofauti hizo zilidhihirika na zikaleta ikhtilafu kati ya watu lakini Nabiy (صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) akatatua tatizo hilo kwa kukiri usahihi wake kama mfano wa tukio alilohadithia 'Umar ibn Al-Khatwaab (رضي الله عنه) ambaye amesema:

سَمِعْتُ هِشَامَ بْنَ حَكِيمٍ بْنَ حِزَامٍ يَقْرَأُ سُورَةَ الْفُرْقَانِ عَلَى غَيْرِ مَا أَقْرَوْهَا وَكَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَقْرَأَنِيهَا، وَكِدْتُ أَنْ أَعْجَلَ عَلَيْهِ ثُمَّ أَمْهَلْتُهُ حَتَّى انْصَرَفَ، ثُمَّ لَبَبْتُهُ بِرِدَائِهِ فَجِئْتُ بِهِ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ فَقُلْتُ: إِنِّي سَمِعْتُ هَذَا يَقْرَأُ عَلَى غَيْرِ مَا أَقْرَأْتُنِيهَا. فَقَالَ لِي: ((أَرْسَلْتُ)) ثُمَّ قَالَ لَهُ: ((أَقْرَأْتُ)) فَقَرَأَ فَقَالَ: ((هَكَذَا أُنْزِلَتْ)) ثُمَّ قَالَ لِي: ((أَقْرَأْتُ)) فَقَرَأْتُ، فَقَالَ: ((هَكَذَا أُنْزِلَتْ، إِنَّ الْقُرْآنَ أُنْزَلَ عَلَى سَبْعَةِ أَحْرُوفٍ فَاقْرَءُوا مِنْهُ مَا تَيَسَّرَ))

"Nilimsikia Hishaam ibn Hakim akisoma Suwratul-Furqaan tofuti na vile ninavyoisoma na alivyonifundisha Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم). Nilikaribia kumsimamisha (asiswalishe) lakini nikamvumilia mpaka akamaliza kisha nikamshika nguo yake shingoni na kumvuta mpaka kwa Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) nikasema: "Nimesikia huyu mtu akisoma (Suwratul-Furqaan) kinyume na ulivyonifundisha." Rasuli wa Allaah (صلى الله عليه وآله وسلم) akasema: ((Mwachie!)) Akamwambia (Hishaam): ((Soma)). Akasoma. Akasema: ((Hivi ndivyo ilivyoteremshwa)). Kisha akaniambia mimi: ((Soma)). Nikasoma. Akasema: ((Hivi ndivyo ilivyoteremshwa. Hakika Qur-aan imeteremshwa kwa Sab'ah Ahruf, hivyo someni iliyokuwa sahali kwenu)) [Al-Bukhaariy, Muslim na wengineo]

Wakati wa ukhalifa wa 'Uthmaan bin 'Affaan (رضي الله عنه), Uislamu ulienea sehemu mbali mbali, na tofauti katika usomaji Qur-aan katika lahaja mbalimbali za lugha ya Kiarabu ulijidhihirisha kiasi cha kuleta ikhtilafu na matatizo. Baadhi ya makabilaa walijisifia kisomo chao jambo lilopelekea kutokea mabishano. Pia Waislamu wapya walitatzwa na kuchanganya kisomo bila ya kujua.

Kikundi cha Maswahaba, kilichoongozwa na Hudhayfah ibn Al-Yamaaniy (رضي الله عنه) ambaye alikuwa Iraq, kilikuja kwa 'Uthmaan (رضي الله عنه) na wakamsihi auokoe Ummah wa Kiislamu kabla haujatofautiana juu ya Qur-aan. 'Uthmaan (رضي الله عنه) akaamrisha chini ya uongozi wa Zayd bin Thaabit (رضي الله عنه) nakala za Qur-aan ziandikwe na nakala zote zisizo rasmi zichomwe moto.

Lahaja iliyotumika kuandika Qur-aan ni ile ya ki-Quraysh na Mswahafu ukajulikana kuwa ni ‘Mswahafu wa ‘Uthmaan’. Nakala hizo zilisambazwa miji mikuu ya Waislamu zikiwa kama *nuskah* (kopi) rasmi. Na *nuskah* ya asili ikabakishwa kwa Mama wa Waumini Hafswah (رضي الله عنها). Alimwacha Zayd bin Thaabit Madiynah, ‘Abdullaah bin Swaa’ib alitumwa Makkah, Mughiyrah bin Shu’bah alitumwa Syria, Abuu ‘Abdir-Rahmaan As-Sulamy alitumwa Kuwfah, ‘Aamir bin ‘Abdil-Qays alitumwa Baswrah.

Baada ya kusambazwa nakala rasmi za ‘Mswahafu wa ‘Uthmaan’, lahaja zote zinginezo zikapotea ikabakia lahaja ya ki Quraysh pekee.

Kwa hiyo Mswahafu ulioko hivi sasa kwa Waislamu ni ule ulioandikwa na kusomwa kwa lahaja ya Quraysh na Viraa-a vyote vinatokana na mfumo huo wa Mswahafu. Hii ni rai ya gurupu la ‘Ulamaa. Wengineo wameona kwamba baadhi ya lahaja zimehifadhiwa katika Viraa-a tofauti lakini ni zile tu zinazokubaliana na Mswahafu wa ‘Uthmaan. Wamesema Maswahaba waliuandika Mswahafu wa ‘Uthmaan (kwa kuondoa vidoto na *i’raab*) ili kuzipa fursa Ahruf (aina) nyenginezo zilolingana kusomeka. Rai hii imetiliwa nguvu na As-Suyuwtwiyy, Ibn Hajar, ibn Al-Jazariyy na ‘Ulamaa wengineo.


Je, Kuna Tofauti Ya Ahruf Sab’ah Na Viraa-a Saba?

Vitu viwili hivi vinatofautiana kabisa. Viraa-a havikujulikana wakati wa Nabiy (صلى الله عليه وآلہ وسلم) na Maswahaba zake. Lakini ikawachanganya watu kudhania kwamba ni kitu kimoja kwa vile idadi ya Ahruf ni Saba na Viraa-a vilonukuliwa katika Shairi Maarufu la Ash-Shaatwibiyyah ni saba.

Viraa-a saba vimetokana na katika mojawapo ya Ahruf Sab’ah ambayo ni lahaja ya Quraysh aliyoichagua ‘Uthmaan. Viraa-a saba hivyo ni kama vilivyotajwa katika ‘Historia ya Elimu ya Tajwiyd na Viraa-a’.

Kuwekwa Vidoto Na I’raab katika Mswahafu:

Mswahafu wa 'Uthmaan haukuwa na vidoto vinavyotofautisha baina ya herufi mfano **ظ ص خ ح ج** n.k. na pia haukuwa na *i'raab* (fat-hah, kasrah, dhwammah), wala haukuwa na namba za Aayah au alama za kusimama, ulikuwa kama ifuatavyo:



Kuisoma Qur-aan katika hali hiyo haikuwa ngumu kwa Waarabu wasomi walioielewa vyema lugha yao. Lakini baada ya watu wa kigeni kuingia katika Uislamu, walitatizwa kuifahamu na makosa yakadhihirika. Tatizo hili lilidhihirika zaidi Iraq. Abul-Aswad Ad-Duwaly (aliyefariki 69 H), alimsikia mtu akisoma Aayah ifuatayo kwa kutamka '*Rasuwlihi*' (kwa kasrah) badala ya '*Raswuluhu*' (kwa dhwammah) jambo linalopeleka kuharibu na kupotosha kabisa maana ilokusudiwa:

..... أَنَّ اللَّهَ بِرٌّ إِنَّمَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ وَرَسُولُهُ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ

.... kwamba Allaah Hana dhima na washirikina na pia Rasuli Wake [At-Tawbah (9: 3)]

Abul-Aswad Ad-Duwaly alipoombwa kwanza kurekebisha Mswahafu kwa kuweka *i'raab* n.k alikhofia kuzusha jambo katika Dini. Lakini kwa vile kosa kama hilo ni kubwa mno linalopotoa maana iliyokusudiwa, lilimsh tua hadi akaamua kuifanyia kazi, ndipo alipoanza hatua ya kwanza kuweka *i'raab*.

